


Septemba 18, 2023

Mch. Almodad Amos

# 01. Faida 5 za Kujifunza Unabii

Majanga ya asili na mizozo ya kisiasa iliyopelekea vita ni vitu ambavyo vinaonekana kwamba vimekuwepo katika historia ya binadamu, na daima vimekua vikisababisha magonjwa na vifo vingi. Litakalokushangaza zaidi ni kwamba katika siku za hivi karibuni, ukubwa na upeo wa matukio haya umeongezeka sana. **Kuanzia mwaka 1990, majanga ya asili yameathiri watu wapatao milioni 217 kila mwaka, na karibu watu milioni 300, hivi sasa wanaishi katika hali hatarishi** kote ulimwenguni. Madhara ya mara moja na ya muda mrefu ya usumbufu huu kwa watu wengi yamepelekea matatizo mengi kwa wanadamu ...

— New England Journal of Medicine, November 7, 2013

... ikiwemo: **Kuporomoka kwa uchumi, mabadiliko ya tabia ya nchi, hali ya kukosekana kwa amani, na hisia kwamba kuna jambo flani kubwa lisilojulikana linalokwenda kuupata ulimwengu huu**.

## Hofu imeendelea kuongezeka

Hofu imeendelea kuwaangukia **wakazi wa dunia hii kila wanapojiuliza nini kitatokea Kesho: Mwisho wa haya magonjwa, vimbunga na matetemeko yanayoendelea kuvunja rekodi kila uchao, umaskini** unaoendelea kukomaa kila siku, **matukio ya kigaidi**! Watu wanahoji: **kesho itakua namna gani?**

## Utabiri wa Nyota

Wengi wanakimbilia utabiri wa nyota wakitaka kujua kesho itakuaje.

## Utabiri wa Kichawi

Wengine wamewakimbilia wachawi bila mafanikio.

## Tafiti za Kisayansi

Wengine wameigeukia sayansi ili kutafuta majibu kwamba kesho itakuwa je!

Utabiri wa nyota, utabari wa kichawi na tafiti za kisanyansi, vyote kwa pamoja haviwezi kuleta majibu ya swali muhimu linaloukabili ulimwengu huu. Mwisho wa mambo haya utakua je? Nini kinafuata baada ya Uviko – 19? Nini mwisho wa mabadiliko ya tabia ya nchi? Je, liko tumaini kweli?

Wengi wameikimbilia pombe, wengine wamejiingiza ktk madawa ya kulenya. Wengi wamepoteza maisha yao na kuamua kujinyonga baada ya kukosa majibu yenye matumaini juu ya mambo ya kutisha yaliyowakabili maishani mwao. Huenda hata na wewe unaweza ukawa unawaza kujinyonga maana umeshindwa kuelewa kesho yako au kesho ya hali inayokukabili itakua je .... Lakini kabla hujafika huko, ninayo habari njema kwako.

## Yesu Kristo Ameifunua Kesho

Habari njema ni Kwamba: Ni Mungu peke yake anayejua vizuri na kwa uhakika juu ya kila tukio litakalotokea ktk siku za usoni. Yeye anajua kila kitu. Yeye ni Mwanzo na Mwisho, Ni Alfa na Omega. Hakuna asichokijua. Hata mambo ambayo yako miaka maelefu huko mbeleni, Yeye anayafahamu sawa-sawa na anavyoifahamu Juzi, jana na leo.

**Kwa habari ya kujua kwake: Kesho yako haina tofauti na leo au jana**. Anaijua vizuri sana na endapo utakubali kumsikiliza utagundua kwamba anao uwezo wa kukutangazia na kukuonyesha mambo yatakayokuwako hivi karibuni.

> Isaya 46:9,10 ... maana **mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi; 10 nitangazaye mwisho tangu mwanzo**, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote.

Hakuna haja ya kujisumbua kwa ajili ya kesho, hakuna haja ya kuwa na msongo kupita kiasi, hakuna haja ya kujinyonga kwa kuogopa yatakayokuja kesho. Hiyo Kesho unayoigopa tayari Mungu amekwisha kuiingia na kama ukimtumaini atakupitisha salama. Cha kufanya ni kumtumaini na kmwamini.

Mungu wetu anayeijua Kesho, amekwisha kuichora na kuiandika Historia nzima ya ulimwengu huu na ameleta kwetu kupitia Kitabu Kinachoitwa Biblia. Biblia ndiyo Kitabu pekee ambacho Mungu aliwapatia wanadamu ili kiweze kuwa ramani na dira isiyokosea, ya kuwaongoza watu katika maisha ya siku kwa siku.

Na miongoni mwa vitabu 66 vilivyomo ktk Biblia, kuna vitabu 2 ambavyo vimetengwa maalum kabisa kwa ajili ya Nyakati zetu, yaani wakati tunaoishi sasa, mpaka tutakapofika katika vilele vya Historia ya ulimwengu huu. Ninazungumzia Kitabu cha Danieli na Kitabu cha Ufunuo.

Ni vizuri daima ukumbuke ahadi ya Mungu:

> Amos 3:7 Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.

## Kwa Nini Tujifunze Unabii?

> Mambo yaliyofunuliwa kwa Danieli baadaye yalitimizwa na ufunuo uliotolewa kwa Yohana kwenye kisiwa cha Patmo. Vitabu hivi viwili vinapaswa kutazamwa kwa uangalifu.
>
> - Manuscript Releases [Nos. 1301–1359, 1987–1988] (Vol. 18, p. 15). (1993). Ellen G. White Estate.

### 01: Kupata amani moyoni katikati ya ulimwengu uliojaa matukio ya kutisha na mambo ya kukatisha tamaa

> 2 Petro 1:19 Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.

Mungu anachofanya katika unabii ni kutufunulia mambo yatakayokuwako kabla hayajatokea, ili wakati yanapotokea tusitishike bali badala yake Imani zetu ziimarike katika Yeye.

### 02: Unabii unatuandaa kushinda na namna ya kukabiliana na dhiki ambayo Shetani ataileta kwa watu wa Mungu

> Ufunuo wa Yohana 2:10 Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.

- **Kwanza**: Zinatajwa mbinu atakazotumia Shetani k.v.: kufungwa gerezani na kuleta dhiki.
- **Pili**: Mbinu inayotajwa ya Kushinda ni Kuwa mwaminifu kwa Mungu.

### 03: Unabii unaweka wazi mahali ambapo mara nyingi watu wamekua wakianguka ili liwe funzo kwetu (ili tusirudie makosa)

> 1 Wakorintho 10:11 Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na miisho ya zamani.

## 04: Unabii ni njia ambayo Mungu huitumia ili kutusaidia kujua mambo ya siku za usoni na matukio yatakayotokea huko mbeleni

> Isaya 46:9 kumbukeni mambo ya zamani za kale; maana mimi ni Mungu, wala hapana mwingine; mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi; 10 nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote.

## 05: Unabii ni njia ambayo Mungu ameichagua, ya kuwajaza matumaini wale wampendao na kuwaandaa kwa miisho yao ya ushindi

Sehemu bora zaidi ya kujifunza unabii inapaswa kuwa mtazamo mpya unaopata baada ya kusoma kitabu cha Agano Jipya cha Ufunuo na Kitabu cha Danieli, hasa sura za mwisho za vitabu hivi.

**Unabii unaonyesha mwisho wa mambo yote haya utakua sawa**. Na hii inatusaidia kuwa wastahimilivu kwa sababu bila tumaini huwezi kuwa mstahimilivu.

> Ufunuo wa Yohana 21:4 Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.

Mungu anachofanya katika unabii ni kutufunulia mambo yatakayokuwako kabla hayajatokea, ili wakati yanapotokea tusitishike bali badala yake Imani zetu ziimarike katika Yeye.

## 06: Unabii unaleta hali ya uamsho wa kiroho katika maisha ya watu wa Mungu na kuwasaidia kuwa na tabia iliyo bora

> Vitabu vya Danieli na Ufunuo vinapoeleweka vyema, waumini watakuwa na uzoefu tofauti kabisa wa kidini. Watapewa vionjo vya malango ya mbinguni yaliyo wazi ili kwamba moyo na akili vivutiwe kuhusiana na tabia ambayo wote wanapaswa kuikuza ili kupata baraka ambayo itakuwa thawabu ya walio safi moyoni.
>
> – Manuscript Releases [Nos. 1301–1359, 1987–1988] (Vol. 18, p. 24). (1993). Ellen G. White Estate.